Mtazamo Dhidi Ya Ndugu Zetu

(Attitude Towards Our Brethren)

Na

Ellis P. Forsman

Mtazamo Dhidi Ya Ndugu Zetu

(Attitude Towards Our Brethren)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Mtazamo Dhidi Ya Ndugu Zetu

Zaburi 100:2-4

Mtazamo mwema kimsingi ni njema. Ni mhimu katika kusanyiko la mahali fulani.

Kidini tunaweza kuwa na mtazamo unaoleta baraka kutoka kwa Mungu, au isiyoleta upendeleo kutoka kwake.

Tulijifunza kuhusu mtazamo wetu dhidi ya Mungu, Yesu Kristo, injili, na kanisa; sasa tutajifunza kuhusu mtazamo wetu dhidi ya ndugu zetu.

Miaka mingi zaidi (hata kutoka katika karne ya kwanza) kanisa limeteseka kwa sababu ya mtazamo mbaya ambao ndugu wamekuwa nayo dhidi ya kila mmoja. Leo tunataka kujadili kuhusu mtazamo mwema dhidi ya kila mmoja, ili kwamba kazi ya Bwana ibarikiwe.

Ebu na tuipe mioyo yetu mitazamo mwema.

Mtazamo wa Upendo

Yesu alitufundisha umuhimu wa kuwapenda ndugu zetu. Yoh. 13:34-35, "*Hayo yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia neno; ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema, nitafumbua kinywa changu kwa mfano, nitayatamka yaliyositirika tangu awali.*"

Upendo kama inavyotafsiriwa katika Fil. 2:3-4, "*Msitende neno lolote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Kila mtu asiangalie nafsi yake mwenyewe, bali kila mtu aangilie mambo ya wengine.*"

Wakristo walio na upendo wa Kristo wanamuangalia kila mmoja wao.

Tumezaliwa kwa mara ya pili ili tuwapende wenzetu pasipo upendeleo. 1 Pet. 1:22-23, "*Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo. Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele.*"

Upendo unajumuisha kujitoa sisi wenyewe katika kutoa muda wetu kwa wengine – na wakati mwingine hiyo hujumuisha hatari. Tunajitoa wenyewe katika kuwasaidia wengine kwa njia yo yote tunayoweza kulingana na hitaji. Tunajitoa wenyewe kuwatia nguvu

wengine. Tuanjitoa wenyewe kuwaelimisha wengine (kuwafundisha). Tunajitoa wenyewe kuwa kemea wengine katika (upendo na upole)

Efe. 4:15, "*Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote yeye aliye kichwa, Kristo.*"

Gal. 6:1, "*Ndugu zangu mtu akighafilika katika kosa lolote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe.*"

Kama kweli tunapendana sisi kwa sisi, tutapenda kuweka wenzetu kuwa wa kwanza.

Mtazamo dhidi ya Ushirikiano

Hii inajumuisha matakwa ya kufanya kazi pamoja, kama Mungu alivyokusudia.

1 Kor. 12:21-27, "*Na jicho haliwezi kuuambia mkono, sina haja na wewe; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu, sina haja na ninyi. Bali zaidi sana vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa vinyonge zaidi vyahitajiwa zaidi. Na vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi; na viungo vyetu visivyo na uzuri vina uzuri zaidi sana. Kwa maana viungo vyetu vilivyo na uzuri havina uhitaji; bali Mungu ameungamanisha mwili, na kukipa heshima zaidi kile kiungo kilichopungukiwa; ili tusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe. Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho. Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila mmoja peke yake.*"

Tunapaswa kuwa na uwezo sio tu wa kufanya kazi, bali pia kufanya kazi pamoja. Efe. 4:16, "*Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila kiungo, kwa kadiri ya kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.*"

Linapokuja swala la kushirikiana na wengine, (hasa kuhusiana na swala linalohusu kazi ya kanisa) je unajiona mwenyewe kama mmoja wa wafuatao?

- Mkono uliovunjikia kwenye rimu?
- Msuguano katika gia?
- Uzito wa ziada?
- Girisi?

- Mafuta?

Isipokuwa kila kiungo kitimize wajibu wao kanisa litatingwa katika kazi yake.

Mtazamo wa Utii

Tunapaswa kuwa watumishi.

- Mat. 23:11, "*Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu.*"
- Luka 22:26, "*Lakini kwenu ninyi sivyo; bali aliye mkubwa kwenu na awe kama aliye mdogo; na mwenye kuongoza kama yule atumikaye.*"

Tunapaswa kujitoa kwa kila mmoja. Efe. 5:21, "Hali mnanyenyekeana katika kicho cha Kristo."

Hasa, tunapaswa kujitoa katika wale waliona nafasi za uongozi Ebr. 13:17, "*Watiini wenye kuwaongoza na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewafaa ninyi.*"

Mfano mbaya. 3 Yohana1:9, "*Naliandikia kanisa neno, lakini Diotrefe, apendaye kuwa wa kwanza kati yao, hatukubali.*"

Diotrefe kila wakati aliharibu nafasi yake.

Utii (utumishi) unaifanya kanisa kuendelea kiulaini.

Mtazamo wa Amani

Lazima tutafute amani na kila mmoja. Rum. 14:19, "*Basi kama ni hivyo na mfuate mambo ya amani na mambo yafaayo kujengana.*"

Ni kutembea vizuri kulingana na wito wetu. Efe. 4:1-3, "*Kwa hiyo nawasihi mimi niliyemfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa; kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani.*"

Kujitahidi – kukazana, kufanya kazi kwa nguvu.

Yakobo 3:17-18, "*Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi, tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki. Na tunda la haki hupandwa katika amani na wale wafanyao amani.*"

Wakati kila mmoja akijitahidi katika imani, tunda ni amani.

Zaburi 133:1, "*Tazama jinsi ilivyo vyema, na kupendeza, ndugu wakae pamoja, kwa umoja.*"

Lakini sio amani kwa sababu tu ya amani. Kuwa na umoja katika kweli ya neno la Mungu. Hatupaswi kutoa dhabihu neno lake kwa ajili ya umoja, lakini kuna mengi ambayo ndugu wanaweza kuwa na umoja nayo – kama vile kufanya maamzi juu ya ujenzi, au kufanya mipangilio ya mkutano.

Njia nyingine katika amani ni maangamizi ya mtu binafsi. Gal. 5:15, "*Lakini mkiumana na kulana, angalieni msije mkaangamizana.*"

Hili linapotokea hakuna kinachokamilishwa na inaonyesha kwamba upendo wa Mungu na wa ndugu zetu haupo katikati yetu.

Mtazamo wa Ukarimu

Wakristo wanatakiwa kuwa wakarimu. Rum. 12:9-13, "*Pendo na lisiwe na unafiki lichukieni lililo ovu, mkiambatana na lililo jema. Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu; kwa bidii si walegevu mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana; kwa tumaini mkifurahi; kati dhiki; mkisubiri katika kusali, mkidumu; kwa mahitaji ya watakatifu, mkifuata ukarimu; katika kukaribisha wageni mkijitahidi.*"

Hii inajumuisha ukarimu kwa wageni na kwa ndugu.

- Ebr. 13:1-2, "U*pendano wa ndugu na udumu. Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.*"
- 1 Pet. 4:8-10, "*Zaidi ya yote iweni na juhudi nyingi katika kupendana; kwa sababu upendano husitiri wingi wa dhambi. Mkaribishane nyinyi kwa nyinyi, pasipo kunung'unika; kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu.*"

Haitufanyii wema wo wote kama tunajisikia kwamba tunapaswa kuwa wakarimu – tunapaswa kutaka kuwa wakarimu.

Sababu za kanisa kusambaa kwa kasi katika karne ya kwanza ulikuwa ni ikarimu uliopanuliwa na Wakristo. 3 Yohana 1:5-8, "Mpenzi kazi ile ni ya uaminifu uwatendeayo hao ndugu na hao wageni nao, waliokushuhudia upendo wako mbele ya kanisa utafanya vizuri ukiwasafirisha kama ipasavyo kwa Mungu. Kwa maana kwa ajili ya jina hilo, walitoka wasipokee kitu kwa Mataifa. Basi imetupasa sisi kuwakaribisha watu kama hao, ili watenda kazi pamoja na kweli."

Ukarimu ni tunda la moyo unaojitoa.

Nia ya Joto, Urafiki, Uwazi

Tunaona msemo huu kwa wale waliokuwa katika kanisa Yerusalemu.

Mdo. 2:44-47, "*Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja na kuwa na vitu vyote shirika, wakiuza mali zao na vitu walivyokuwa navyo na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja. Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*"

Na ikaendelea kwa watakatifu katika Antiokia.

Mdo. 11:27-30, "*Siku zizo hizo manabii walitelemka kutoka Yerusalemu hata Antiokia. Na tulipokusanyika akasimama mmoja wao, jina lake Agabo, akaonyesha kwa uweza wa Roho Mtakatifu kwamba njaa kubwa itakuja karibu katika dunia nzima nayo ikatukia katika siku za Klaudio. Na wale wanafunzi kila mtu kwa kadri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokuwa Uyahudi. Wakafanya hivyo, wakawapelekea wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli.*"

Wakati mtu yupo katika hitaji kwa sababu ya ajali, moto, au janga la kitaifa, tunaitaji kuwapa cho chote kinachohitajika. Wakati mwingine hivyo inaweza kumanisha sadaka kwa upande wetu.

Mtazamo wa Msamaha, Kuchukuliana, Upole, Uvumilivu

Mitazamo yote hii huingiliana, na ni muhimu sana.

- Efe. 4:2, "*Kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu mkichukuliana katika upendo.*"
- Efe. 4:32, "*Tena iweni wadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*"

Wote tunahitaji kusamehewa. Sote tunahitaji wengine kuchukuliana nasi. Sote tunahitaji wengine kuwa wapole dhidi yetu. Sote tunahitaji wengine watuvumilie.

Kama jinsi sisi kila mmoja anavyohitaji vitu hivi tufanyiwe katika maisha yetu, kumbuka kwamba wengine pia wanahitaji vitu kama hivi kutoka kwetu pia.

Vitu kama hivyo usaidia kulainisha miinuko na vikwazo ambavyo Shetani anaweka mbele zetu katika juhudi zake za kuhangamiza kanisa la sehemu moja.

"Imebarikiwa Kifungo Ambacho Hufunga"

Tunafurahia baraka ya ajabu katika Kristo katika ushirika wetu na Wakristo wengine. Sisi ni kiungo kwa kila mmoja. Rum. 12:5, "*Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo kila mmoja kwa mwenzake.*"

Hivyo tuna mfungamano wa kipekee au kifungo kinachotufunga pamoja.

Wimbo ulio rahisi alafu nzuri unaoelezea mfungamano huu ni "Imebarikiwa Kifungo Kitufungacho". Maneno hayo yaliandikwa na John Fawcett katika mwaka wa 1782. Lakini ladha iliwekwa na Johann G. Nageli, na kupangwa na Lowell Mason katika mwaka wa 1845.

Kutoka katika maneno ya wimbo huu, tuchukue nafasi hii kuangalia kifungo hiki cha kipekee tunachokifurahia kama Wakristo.

Aya ya kwanza. "Imebarikiwa kinachofunga mioyo yetu katika upendo wa Kikristo."

Zingatia sasa kwamba kifungo kinachofunga katika upendo ambao hauvunjiki kirahisi. Kol. 3:14, "*Nakaza mwendo niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.*"

Upendo unaotoka kwa Mungu wa upendo. 1 Yohana 4:7-11, "*Wapenzi na mpendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. Yeye asiyependa hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo. Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni ili tupate uzima kwa yeye. Hili ndilo pendo si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi*

zetu. Wapenzi ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi tupendane."

Ni upendo ndio unaotumika kama alama ya mwanafunzi wa kweli. Yohana 13:34-35, "*Amri mpya nawapa mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.*"

Kifungo kinachojumuisha upendo ni Ukristo wa kipekee; na ni mfano katika upendo wa Kristo.

"Ushirika wa mawazo yaliyotulia ni kama ile iliyoko juu."

Kifungo hiki kinajumuisha umoja ambao Yesu aliomba kwalo. Yohana 17:20-23, "*Wala si hao tu ninao waombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja, ili ulimwengu ujue ya kuwa wewe ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi.*"

Hivyo tishio lolote la umoja huu unakemewa kwa nguvu zote. 1 Kor. 1:10, "*Basi ndugu nawasihi kwa jina Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.*"

Kifungo kinaangalia kuigiza umoja kati ya Baba na Mwana. Kifungo kinachofungaq hutegemea juu ya upendo na umoja ambao Kristo anafanya liwezekane; inaonyeshwaje inaonyeshwa katika aya zilizobaki za wimbo.

Aya ya pili. "Mbele ya kiti cha enzi cha baba yetu tunamimina sala motomoto."

Tumebarikiwa kuweza kuwa tayari kumkaribia Mungu katika sala. Hii ndiyo nafasi tunayoifurahia katika Kristo.

Ebr. 4:14-16, "*Basi iwapo tuanaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hakuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*"

Ni nafasi na baraka kuu. Ebr. 4:16, "*Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*"

Wimbo huu unaonyesha maombi ya muda wote na maombi ya kina.

Kuwaombea kila mmoja

Yakobo 5:16, "*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa. Na kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii.*"

Kuomba na mwingine

- Mdo. 2:42, "*Wakawa wakidumu katika fundisho la Mitume, na kati*ka ushirika,na katika kuumega mkate na katika kusali."
- Mdo. 21:5, "*Hata tulipotimiza siku zile tukaondoka tukaenda zetu, na watu wote, na wake zao, pamoja na watoto wao, wakatusindikiza mpaka nje ya mji, tukapiga magoti pwani tukaomba.*"

Maombi kama haya ni faida ya kifungo kinachofunga, na pia huutia nguvu kifungo hicho.

"Uoga wetu, taraja letu, kusudio letu ni moja, faraja letu na kujali kwetu."

Tuna kujali kunakofanana na hamu. Baadhi kwa sababu sisi ni wanadamu katika dunia. Tunahamu ya kuwa na afya, tunaogopa magonjwa na kufa. Tunafurahia faraja la uzima, tunaogopa kutokuwa na kazi na umasikini. Tunania zinazofanana kwa sababu sisi ni raia wenza wa ufalme.

Tunashiriki tumaini la ufufuo na uzima wa milele. 1 Pet. 1:3, "*Ahimidiwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu;*"

Tunashiriki katika jitihada dhidi ya majaribu na mateso. 1 Pet. 5:8-9, "*Mwe na kiasi na kukesha kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye huzunguka zunguka akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo mkiwa thabiti katika imani mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani.*"

Hivyo basi, kama Wakristo tunaweza kushiriki mengi; siyo tu kwa sababu ya asili yetu ya kibinadamu, lakini pia kwa sababu sisi ni washiriki uasili wa kipekee.

Neema na amani huzidishwa. 2 Pet. 1:2-3, "*Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu. Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo*

uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe."

Tuna ukuu mkuu na ahadi nzuri. 2 Pet. 1:4, "*Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.*"

Ujuzi wetu ulioshikiwa, urithiwa na baraka zetu za kiroho, huipa nguvu kifungo chetu. Kifungu kinachofuata uangazia matatizo ambazo wakati fulani tunakabiliana nazo.

"Mzitari wa tatu. Sote tunashiriki maonyo, mizigo yetu tunayobeba."

Kama Wakristo, tunapaswa kubeba mizigo ya kila mmoja. Gal. 6:1-2, "*Ndugu zangu mtu akighafilika katika kosa lolote, ninyi mlio wa Rohoni mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe. Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.*"

Katika nyakati za udhaifu wa kiroho, tunapaswa kumuombea kila mmoja. Yakobo 5:16, "*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii.*"

Katika wakati wa mateso, tunapaswa kumkumbuka kila mmoja. Ebr. 13:3, "*Wakumbukeni hao waliofungwa kana kwamba mmefungwa pamoja nao; na hao waliodhulumiwa, kwa vile ninyi nanyi mlivyo katika mwili.*"

Katika wakati wa mahitaji ya kimwili, tunapaswa kusaidia kila mmoja. Yakobo 1:27, "*Dini iliyo safi isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.*"

Huonyeshwa katika njia, kifungo tulichonacho katika Kristo hakika ni baraka.

"Na mara zote kwa kila mmoja machozi ya huruma hutiririka."

Kwa sababu hivyo ndivyo Mungu alivyouunganisha mwili wa Kristo! 1 Kor. 12:24-26, "*Kwa maana viungo vyetu vilivyo na uzuri havina uhitaji; bali Mungu ameuungamanisha mwili, na kukipa heshima zaidi kile kiungo kilichopungukiwa; ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe. Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho.*"

Ili tulie na wale wanaolia. Rum. 12:15, "*Furahini pamoja na wafurahio; lieni pamoja nao waliao.*"

Ni hisia lakini ni muonekano thabiti wa kifungo tunacho shiriki.

Kifungu cha mwisho kinaelezea mshikamano wa kifungo kinachofunga, inapokuja wakati wa kutengana, hata kwa muda.

Kifungu cha nne. "Tunapotengana inatupa maumivu ya kindani."

Kifungo ni kile ambacho kikiondoka inaweza kuuma.

Kumbuka mfano wa Paulo na wazee wa Efeso. Mdo. 20:36-38, "*Alipokwisha kunena haya akapiga magoti, akaomba pamoja nao wote. Wakalia sana wote, wakamwangukia Paulo shingoni, wakambusu busu, wakihuzunika zaidi kwa sababu ya neno lile alilosema, ya kwamba hawatamwona uso tena. Wakamsindikiza hata merikebuni.*"

Sijawahi kupata maumivu kama haya? Labda mtu atahitaji kuchunguza kifungo chake.

"Lakini tutaunganishwa ndani ya roho, na kutarajia kukutana tena."

Tunaweza kutenganishwa katika mwili, lakini tunaweza kuwa pamoja kiroho. Kol. 2:5, "*Ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika.*"

Tunafarijiwa na tumaini la ajabu.

Tumaini la ufufuo. 1 Thes. 4:13-18, "*Lakini ndugu hatutaki mjue habari zao walio lala mauti msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao walio lala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi farijianeni kwa maneno hayo.*"

Je tumaini hili linaloweka roho zetu kuungana pamoja, wakati vifungo vingine vyote vinaposhindwa.

Hitimisho

Hebu na tukumbushwe tena kwamba karama zote duniani haziwezi kushinda mitazamo mibaya.

Mitazamo mibaya husababisha matatizo mengi kuliko maswala ya kimaandiko.

Hebu kila mmoja wetu awe na mtazamo wa upendo dhidi ya ndugu, na kujitahidi kwa umoja.